



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MBUNGE JIMBO LA MSALALA

S.L.P 16 – MSALALA

Simu: 0758279707/0689331941

Email: ofisiyambungemsalala@gmail.com

TAARIFA KWA UMMA.

Mbunge wa Jimbo la Msalala Mhe.Iddi Kassim Iddi anapenda kuwafahamisha kuwa Ofisi ya Mbunge kupitia Taasisi yake ya Msalala Foundation imepata ufadhili wa kusomesha mabinti wa kike 50 waliokatisha masomo yao kwa sababu za ujauzito na ndoa za utotoni kupitia progam ya "ELIMU HAINA MWISHO". Ufadhili huo ni wa kwenda kusoma fani mbalimbali chuo cha maendeleo ya wananchi Msanginya kilichopo wilaya ya Mpanda Mkoa wa Katavi. Kozi hizo za zitaambatana na masomo ya Sekondari ya miaka miwili (QT) lengo Ni kumuwezesha mtoto wa kike aweze kupata elimu ya kidato cha nne na fani kwa wakati mmoja. Aidha, masomo yataanza tarehe 22.01.2023

FANI ZITOLEWAZO

- Uashi (masonry and Bricklaying)
- Umeme wa majumbani (electrical installation)
- Useremala (carpentry and Joinery)
- Ushonaji na kudarizi (designing sewing cloths technology)
- Kilimo (field and horticultural crops)
- Upishi (food production)

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe ni Binti wa miaka 15- 25.
2. Awe amekatisha Masomo Kwa sababu ya ujauzito na ndoa za utotoni.
3. Aje na barua ya uthibitisho kutoka Kwa Shule aliyosoma.
4. Aje na Barua ya utambulisho na uthibitisho kutoka Kwa Afisa Mtendaji wa kijiji au kata anayotoka.

Maombi yote yanatakiwa yawasilishwe Ofisi za Mbunge zilizopo Kata ya Isaka na Kata ya Segese kuanzia tarehe 20.10.2022 mpaka tarehe 20.11.2022.

ADA NA MALAZI KIPINDI CHOTE CHA MASOMO NI BURE KABISA.

Kwa maelezo zaidi: 0758279707/0623228205

Imetolewa na
Edson J. Erasto
Katibu wa Mbunge,
Jimbo la Msalala.

